# Bei ya kondoo, mbuzi yapanda

Na David Geke

BEI ya mbuzi na kondoo katika machinjio ya Vingunguti, Dar es Salaam imepanda kwa wastani wa Sh 30,000 kwa kila mfugo kutokana na kuongezeka mahitaji kuelekea Sikukuu ya Iddi El Adh'haa ambayo itakuwa keshokutwa.

Mbuzi aliyekuwa anauzwa Sh 120,000 awali, sasa anauzwa Sh 150,000 mpaka 160,000, beberu mkubwa aliyekuwa akiuzwa Sh 160,000, bei yake imefika Sh 300,000. Kondoo aliyekuwa akiuzwa kwa Sh 100,000 mpaka Sh 120,000 kwa sasa anauzwa Sh 130,000 mpaka Sh 140,000.

Akizungumzia biashara hiyo, Mweka Hazina wa Kikundi cha Wauza Mbuzi na Kondoo Vingunguti cha Chiriwaa, Hamisi Ngwangwala alisema bei kwa sasa zimepanda kutokana na wateja kuongezeka wanaofuata mifugo hiyo kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Idd inayowataka wachinje mifugo ikiwa ni kafara wanayotoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Alisema licha ya upandaji huo wa bei, biashara bado ipo vizuri na wanapata wateja hadi wa nje ya nchi.

"Wateja kutoka Comoro wapo, mtu anakuja na kuchukua mbuzi 100 mpaka 150 na wanazidi kuongezeka kadri sikukuu inavyokaribia," alisema.

Mfanyabiashara wa mbuzi, Sudi Bunga alisema kwa sasa uhitaji ni mkubwa katika mikoa wanayochukulia mifugo hiyo ambayo ni Tanga, Morogoro, Manyara na Dodoma.

"Kwenye mikoa hiyo kuna wafanyabiashara wa Kenya pia wanakwenda kuchukua mifugo na kusababisha bei kupanda zaidi," alisema.

## Dawasa yatekeleza mradi mkubwa Chanika

## 'Washtakiwa ni watumishi wa JWTZ